# KUKUA KIROHO

UKRISTO NI MTINDO WA MAISHA, JIFUNZE JINSI YA KUWA MKRISTO WA HAPA DUNIANI

TOLEO LA 001 NOVEMBA 2025 JARIDA MTANDAO - BURE



# UKRISTO WA MAZOEA

JIFUNZE TAFAKURI YA UKRISTO WETU NA MAISHA YETU YA KILA SIKU.

## Mambo ya kuzingatia

Unapookoka hauwi mwana wa Mungu moja kwa moja

## Makosa ya sasa

Huu sio wakati wa TOBA

Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; **basi pendo ndilo utimilifu wa sheria.** '

# YALIYOMO


Utangulizi 02

Somo 03

Makosa ya sasa 05

Ushuhuda 06

Ushauri 08

Maboresho 10

Mambo ya kuzingatia 12

Kukua Kiroho 16

# Utangulizi

Kama taifa tumepita kwenye kipindi kigumu siku ya tarehe 29/10/2025 tumeshuhudia Tanzania mpya ambayo wengi wetu hatukutarajia kama ipo siku na sisi tutakuwa kwenye hali kama tuliyoishuhudia.

Ikiwa ni siku muhimu ya kutumia demokrasia ya kupiga kura kuchagua viongozi wa nchi kwa nafasi ya Udiwani, Ubunge na Rais wa nchi, lakini pia ikawa ni siku ya maandamano ambayo yalipelekea vijana wengi kuuawa, bado hatuna taarifa rasmi ya idadi yao lakini ilikuwa ni siku ngumu na na baadae zilizofuata, ambazo hofu ukimya na uoga ulitawala walioko ndani ya nchi.

Hata sasa tunajifunza kuirudia ile amani yetu na taratibu za zamani lakini kuna mahali matukio yanajirudia kichwani haikuwa siku nzuri kibinadamu kabisa. ambapo kupitia matukio hayo ndio somo likapatikana WAKRISTO tunaosali tulikuwa wapi hadi kuruhusu haya yote kutokea, Je ni kweli kwamba hatukuombea Amani? hatukuombea kumalizika salama? kama tulifanya kwanini **YAMETOKEA**

# UKRISTO WA MAZOEA

Kama taifa tumepita kwenye kipindi kigumu siku ya tarehe 29/10/2025 tumeshuhudia Tanzania mpya ikiwa ni siku muhimu ya kutumia demokrasia ya kupiga kura kuchagua viongozi lakini pia ikawa ni siku ya maandamano ambayo yalipelekea vijana wengi kuuawa, bado hatuna taarifa rasmi ya idadi yao lakini ilikuwa ni siku ngumu na zile baadae zilizofuata, hata sasa tunajifunza kuirudia ile amani yetu na taratibu za zamani lakini kuna mahali matukio yanajirudia kichwani haikuwa siku nzuri kibinadamu kabisa.

Lakini nikapata nafasi ya kujitafakari, kwanini imetokiwa na ikiwa tuliomba na kufunga kwa ajili ya amani na kupita salama?

1.Hatukuombea uchaguzi ? ( Tuliomba)
2.Hatukuombea amani ? ( Tuliomba)
3.Hatukuombea machafuko? ( Tuliomba)

Swali likabaki kwanini yametokea kinyume na maombi yetu?

1.Mungu ametujibu?
2.Kuna unabii uliotimia?
3.Ulisikia nini kipindi cha kuomba kama mwongozo wa kupita salama kipindi hiki?

**Kumbukumbu**
**29/10/2025**

# UKRISTO WA MAZOEA

Hapa ndio nikagundua kuna mahali kuna shida ila bado tunairuka na kuona tuko sawa, somo hili ni kwa ajili ya kukukumbusha eneo lako kwa hadhi yako na sio kwa maana nyingine, tunatofautiana viwango vya imani kuna mwingine anaweza kusema, linatoka ili kujionyesha imani HAPANA lakini uhalisia lazima usemwe.

Ikiwa tulifanya vyote na bado yakatokea, hapo shida iko kwa nani ( *MUNGU au sisi*), jawabu ni sisi, tofauti kati ya jibu na jawabu ni kwamba jibu ni lolote lakini jawabu ni sahihi, Mungu wetu sio mwanadamu wala hayuko kwenye hadhi ya kumlinganisha na mwanadamu sababu miisho na ukuu wake sisi hatuwezi hata kuufikiria acha kufanya hata kufikiria, yaani kiwango chetu cha mwisho sisi kuwaza(akili) ndio yeye anapoanzia.

Je ni makosa yetu kwenye kufanya au alitujibu ila hatukumuelewa Mungu?

Bado nikaendelea kupata maswali na fikirishi maana inaweza kuwa hatukuomba ipasavyo kwa kuwa hatujui,

> *'Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. '*
> *Rum 8:26*

au tuliomba ipasavyo na Mungu akatujibu ila hatukuyaelewa majibu, maana hatukujiandaa na haya ila tuliyaombea yapite kushoto na amani idumu. Kuna mahali kama wakristo tunafeli na bado tunaendelea pale tulipoishia lakini uhalisia.

# Makosa ya sasa

## MISTARI YA KUJIFARIJI

Huu sio muda wa kutumia mistari ya kujifariji, ilhali ni muda wa kuwa kazini kupambania imani, huu ni muda wa imani kufanya kazi kwa ukubwa wake ( Matendo ya imani kupitia msingi mkuu UPENDO) ni muda wa sura zote za upendo kuonekana ( unaovumilia na unaadhibu).

*'Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye. ' Ebr 12:6*

---

## TUTAMBUE MABADILIKO YA ZAMA

Tutambue mabadiliko ya zama na nyakati, zama za agano la Kale katika nyakati kama hizi ndio hunyanyuka manabii waliotumwa na Mungu na kusimama kwa ajili ya kuliponya taifa, Je zama hizi bado tunatumia mfumo huu?

---

## WEWE NI KUHANI ?

Agano jipya kila mtu ni kuhani( 1 Petro 2 : 9) na hakuna kuhani asiekuwa mlawi hivyo sisi sote ni walawi na pia tunasimama kwa cheo cha ukuhani , hivyo unabii wa siku zako uko pamoja na wewe na maisha yako sio halaiki, msikilize Mungu.

*'Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ' 1 Pet 2:9*

# Ushuhuda

Je wapo wenye shuhuda kupitia hili ?, usitoe shuhuda ya jinsi ulivyojificha ila shuhuda ya maombi kabla ya kutokea, shuhuda za ulivyojihifadhi ni nyingi lakini ndicho ulicho ombea? Shuhuda kabla ya tukio inadhihirisha majibu ya moja kwa moja na sio uokozi wa baadae.

Mimi ninayo ya kwangu sikiliza kwa makini, mimi nilimsikia Mungu kwa eneo na nafasi yangu na sikuombea tahadhari za kuchukua ila Roho Mtakatifu alisema na mimi ikiwa ni kama muongozo na neno likitoka kwa Roho linajaa kwenye utu wako wa ndani ( Nafsi na Roho ) kisha inabaki kazi yako kuuaminisha mwili kuwa kilichosema ni sahihi, mimi neno lilinijia zaidi ya mwezi mmoja kabla na moyo, nafsi akili na roho vikakubaliana ni SAWA, na ilikuwa ni tahadhari ya kuwa siku ya uchaguzi haitapita salama, hivyo nijiandae kwa mambo ya usalama na chakula, nilifanya hivyo kwa nafasi yangu na nilijiandaa vipi.

## Tahadhari nilizochukua

1.Nilinunua chakula ambacho kingeweza kutumika walau mwezi 1 na nusu ama miwili.

2.Nilijiandaa kwa usafiri, hili lilikuwa ni wimbo ulioko kichwani kwa muda wote kuweka mafuta ya kutosha kwenye usafiri, nilifanya ( FULL TANK) na katika hili ni kwamba ikiwa hali haitakuwa shwari kwa siku 3 basi nitaondoka na familia nitasogea Morogoro vijijini ambako huko hakutakuwa na shida, sikuwa na sababu maalum ya kusema Morogoro ila niliamini hivyo.

Habari hizi nilijitahidi kushirikisha watu wangu wa karibu na wale niliopata nafasi ya kuwasiliana nao na kama tulizungumzia tahadhari, na siku yenyewe kila kitu kilikuwa tayari nikawa ndani huku nasubiri imani kufanya kazi.

## Udhihirisho

1. Ni kweli hatukupita salama
2. Morogoro palikuwa salama
3. Gharama za vyakula kupanda baada ya utulivu
4. Gharama za mafuta kupanda
5. Hazikufika siku 3 hivyo niliendelea kubaki nilipokuwa

Uhalisia wa ukristo ni kazi kuamini kile hujakiona, lakini ni kazi zaidi kukifanyia kazi kile ambacho hujakishuhudia, nilifanya shopping ya gharama kubwa ambapo hivyo fedha ilikuwa na matumizi mengine kabisa, lakini kusikiliza na kutii. Kipindi napokea na kufanya ilikuwa kwa imani na tahadhari sikuwaza moja kwa moja kama ni Mungu lakini baadae katika, tafakari ndio nikamsikia Roho na mistari niliyoletewa ni

*1.' Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Mithali 3:5*

*2.'Ndipo BWANA akaniambia, Umeona vema, kwa maana ninaliangalia neno langu, ili nilitimize. ' Yer 1:12*

Hapo ndipo nikagundua sio kwa akili zangu na Bwana aliniambia na neno lake likatimia maishani mwangu na wale niliowaambia kisha wakafanya, japo lilipita ila tahadhari ilitulinda na yajayo baada ya kipindi cha mpito.

Huyo ni mimi jinsi nillivyo mshuhudia Mungu kwenye maisha yangu kupitia tahadhari, sasa wewe Je ulimsikiaje na alisema nini na wewe ambacho kinakudhihirishia kuwa Mungu yupo na anakusikia kila siku, usiseme uhai sababu ameshakupa na siku amekuandikia, jinsi unavyoutunza uhai wako ndivyo utakavyozifikia siku zako ukitunza vibaya hautafika.

Jambo la msingi huu sio muda wa kujifariji kwa kusema kuwa Mungu kuna jambo anaenda kutenda kwa ajili ya kanisa, au ameshatenda ni kutimia tu au Mungu analiandaa kanisa kupitia hili, tupate majibu ya uhakika na Roho Mtakatifu ndani yako akushuhudie, usiseme kwa sababu ya kujipa tumaini au moyo Je ni kweli tunaandaliwa lakini kama tunaandaliwa kwa kitu gani? Na pia huu ni unabii wa nani? Haya ni maswali muhimu sana tukiamua kutoka kwenye kichaka cha kujifariji kwa kila jambo na kuzifanya imani zetu kudumaa na kuanza kukua na kusimamia mambo.

## Kwa kuona kwangu mimi huu ni muda wa kanisa kujiuliza kwanini tumefeli?.

Ikiwa kwa imani ndogo kama punje ya haradali mkuyu unatii kwenda kupandwa baharini, je kwa umoja na maombi yetu tulishindwa kubadilisha majira? Damu ikawa amani? Kwanini sisi tumeshindwa kuzuia machafuko na tuliomba sana hata wengine kufunga?

*'Bwana akasema, Kama mngekuwa na imani kiasi cha chembe ya haradali, mngeuambia mkuyu huu, Ng'oka, ukapandwe baharini, nao ungewatii. ' Lk 17:6*

Ni aidha hatujamsikiliza Mungu au hatujui bado jinsi ya kutumia mamlaka yetu, huu ni muda wa mtu mmoja mmoja na kanisa kwa ujumla kujiuliza Je ulimsikia Mungu katika tabu zako?

**Kanisa**

1. Kwanini kwa umoja wetu hatujafanikiwa ( Imani)
2. Nafasi yetu katika zama hizi iko wapi na tunaitendea haki?

**Mtu.**

1.Unayo imani inayofanya kazi ( kumtumia Mungu)

2.Unamuamini Mungu au unamtumainia?

3.Uliomba? Kama uliomba majibu yako yakoje?

4.Ulimsikia Mungu au mazoea?

5.Unajua kuomba?



**Sehemu za kufanyia kazi.**

1.Jitambue Mkristo na uzijue haki zako ( ahadi ) ziko ahadi za wana wa Mungu na watu wote pia ahadi kwa mtu na taifa, zitambue na uone utofauti wake na wewe unatakiwa kutumia zipi, bila kusahau ahadi za agano la kale na agano jipya.

2.Viwango vya mkristo hadi kuwa mwana (Rum 8 : 29 -30)

*'Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza. 'Rum 8:29-30*

3.Jinsi au namna sahihi ya kuomba ( 1 Tim 2:1

*Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; ' 1 Tim 2:1*

4. Silaha zako mkristo na kuzitumia ( Efeso 6:10-20)

*'Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote; pia na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kwa kufumbua kinywa changu, ili niihubiri kwa ujasiri ile siri ya Injili; ambayo kwa ajili yake mimi ni mjumbe katika minyororo; hata nipate ujasiri katika huyo kunena jinsi inipasavyo kunena. ' Efe 6:10-20*

## 5. Mahusiano yako na Roho Mtakatifu (Yohana 14 : 15 -18, 26)

*Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu. ' Yn 14:15-18*

*'Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia. ' Yn 14:26*

Mungu hajibu kwa halaiki kama ilivyokuwa Agano la kale sasa hivi anatimiza agano lake kwa mtu mmoja mmoja, wokovu ni wa mtu binafsi, unao wajibu wa kuwa mwanamaombi kuwa na uhusiano wa karibu zaid na Mungu, hata katika hili Mungu amewajibu walio wake.( Rum 8 : 28) unaweza kuwa uko kanisani lakini unalitambua kusudi? Umeitwa kwa kusudi la nani la kwako au la kwake?

*'Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. ' Rum 8:28*

## Maboresho:

Kikawaida hapa ndio kipindi ambacho wakristo wengi hukimbilia kufanya mambo kwa mazoea badala ya kumsikiliza Mungu anasema nini kwa wakati husika, ( Hosea 4:6) watu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa.

*'Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako. 'Hos 4:6*

**Huu sio muda wa:-**

**1.Toba** – Sio kosa kutokumsikia Mungu hadi uombee tona na pia sio kosa kuokoka lakini bado hamjui Mungu umemkariri, kuwa navyo ni faida kwako ila kutokuwa navyo kunaondoa faida na urithi hivyo athari ni zako binafsi, wanafunzi waliposhindwa kutoa pepo hawakuomba ila walitafuta maarifa ( Mathayo 17 : 14 -21)

**2.Kufunga** – Ikiwa tuliomba na kufunga na hatukupata majibu kama tuliyotarajia na hatukupata ufunuo wa kwanini, Je ni kwanini tunarudia makosa yale yale tujifunze kwanza kuomba kwa ufasaha ili maombe yetu yawe na maana mbele za Bwana.

Huu ni muda wa kutafakari na kuutafuta uso wa Mungu, mtu mmoja mmoja kwa maana unaokoka wewe kwa imani yako, sio wewe kwa imani ya jirani yako.Ni muda sahihi wa wakristo kukua kiroho kutoka uchanga kwenda kwenye chakula kigumu, ni muda wa kutafakari na kupokea maarifa sahihi. Jaribu hupita ili kukuimarisha au kukushusha imani ukisimama unakuwa imara likikupiga imani yako inashuka, hili lililopita litufundishe kujitafakari na kujipima kuona imani zetu zina matokeo na nguvu kwa kiasi gani.

1.Kuamini
2.Kujitambua kwa hadhi
3.Kumjua Mungu na tabia zake ( Ayubu sura 4 - 27)
4.Kumfuata Mwana ( Njia) ( Soma injili na kuzeielewa)
5.Matendo na Mahusiano ( Kwa muongozo wa Roho Mtakatifu)

**TAMBUA.**

Ukristo sio jina ni mtindo wa maisha, ni muda wa kuufanya huu mtindo wa maisha kuwa sehemu ya maisha yako, tumefungwa kwenye kifungo cha UPENDO( Kol 3 : 14) AMANI ( Efe 4:3) NA HAKI ( Rum 3 :28).

*'Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu. ' Kol 3:14*

*'na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. ' Efe 4:3*

*'Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria. ' Rum 3:28*

# Mambo ya kuzingatia

## AMRI KUBORESHWA

*' Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria. '*
*Rum 13:8-10*

## MSINGI WA UKRISTO : TUNDA LA ROHO

*' Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho. Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana.' Gal 5:22-26*

## TUMEPEWA UWEZO KUFANYIKA WANA

*'Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; ' Yn 1:12*

## MWANA WA MUNGU NI YUPI:

*'Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Rum 8:14*
*'Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; ' Rum 8:16*

# Mambo ya kuzingatia

## SIFA ZA MKRISTO

*' Pendo na lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema. Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu; kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana; kwa tumaini, mkifurahi; katika dhiki, mkisubiri; katika kusali, mkidumu; kwa mahitaji ya watakatifu, mkifuata ukarimu; katika kukaribisha wageni mkijitahidi. Wabarikini wanaowaudhi; barikini, wala msilaani. Furahini pamoja nao wafurahio; lieni pamoja nao waliao. Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi. Msinie yaliyo makuu, lakini mkubali kushughulishwa na mambo manyonge. Msiwe watu wa kujivunia akili. Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote. Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote. Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa, Kisasi ni juu yangu mimi; mimi nitalipa, anena Bwana. Lakini, Adui yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu, mnyweshe; maana ufanyapo hivyo, utampalia makaa ya moto kichwani pake. Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema.'*

*Rum 12:9-21*

# Mambo ya kuzingatia

## MAMBO YANAYOHARIBU UKRISTO WAKO

*'Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. ' Rum 8:6-8*

*'Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia, basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru. Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake.' Rum 13:12-14*

*'Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka. Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria. Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu. ' Gal 5:16-21*

*' Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, Wamekwisha kupata thawabu yao. ' Mt 6:5*

# Mambo ya kuzingatia

## MAMBO YANAYOHARIBU UKRISTO WAKO

*' Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali. ' Mt 6:24*

*' Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba. ' Kol 3:5-10*

*' Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho. Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa. ' 1 Pet 2:11-12*

*'Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele. ' 1 Yoh 2:16-17*

Huu ni muda wa kujitafakari na kuchukua hatua katika kukuza kiwango cha ukristo wako usibaki pale pale siku zote, imani yako inahitaji kukua kwa kuonekana na maombi yako yanatakiwa kudhihirika kwa macho ya nyama pia, ushuhuda uonekane maana sisi ni barua.

# Kukua Kiroho

Kukua kiroho ni huduma ya mafundisho, kukuza na kulea imani kwa mkristo, nia na lengo la huduma hii ni kumsaidia asiekuwa mkristo, anaeingia na kuanza kuwa mkristo, alie mkristo ( mchanga  au aliekomaa) kuweza kutambua maana, mafundisho na kujitambua mwenyewe kupitia  mafundisho hayo.

**KUKUA KIROHO NI WAJIBU WA KILA MKRISTO**

'Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu; ' 1 Pet 2:2

' Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, ' 1 Kor 3:1-2

'Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.' Ebr 5:12-14

Mkristo unao wajibu wa kukuza na kupandisha imani yako kutoka utoto uchanga kwenda utu uzima, uwe na imani yenye uwezo wa kupingana na nguvu za giza bila kuomba ila kwa nguvu zake, kuomba bila kukoma haimaanishi muda wote uwe unaomba tu ila muda wote uwe na muunganiko mzuri kati yako na ulimwengu wa roho kupitia Roho Mtakatifu, hivyo ukiwa na muunganiko huo ni sawa na kuwa kwenye maombi muda wote kwani huko kuna UWEZA , Hekima na Maarifa ambavyo vitakusaidia sana kufanikisha mambo yako katika ulimwengu wa mwili.

Karibu tujifunze kwa pamoja, karibu KUKUA KIROHO.

# JARIDA LA KUKUA KIROHO

NOVEMBA 2025

**Limeandaliwa na**
Elisha Chuma
*Huduma ya Kukua Kiroho*

kukua kiroho
kukua kiroho
kukuakiroho@echu.co.tz